JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
.....
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

,

TAARIFA YA IDARA YA ARDHI NA MALIASILI JULAI 2018

A

UTANGULIZI: Idara ya ardhi na Maliasili ina vitengo viwili ambavyo ni ardhi na Maliasili.

Kitengo cha Ardhi kina sehemu kuu nne ambazo ni Mipango Miji, Upimaji na ramani, uthamini na maendeleo ya ardhi. Kitengo kina wataalam 3 tu (afisa ardhi Msaidizi na Warasimu Ramani Wasaidizi 2) ambapo mahitaji ya kitengo ni wataalam 12 (Afisa Ardhi Mteule 1, Afisa mipango 1, wapima 3, Warasimu ramani 2, Mthamini 1 na Maafisa ardhi wasaidizi 4).

Kitengo cha Maliasili kina wataalam 3 (Afisa Ardhi na Maliasili, Afisa Maliasili na Msaidizi Misitu) ambapo mahitaji ya kitengo ni Afisa Misitu Wilaya 1 Maafisa Misitu 2, Wasaidizi misitu 4, Afisa Wanyamapori Wilaya 1, Maafisa Wanyamapori Wawili na Afisa utalii mmoja

Upungufu huu umetokana na kutoletewa wataalam mbadala baada ya baadhi ya wataalam kufariki Dunia, wengine kuhamishwa na Halmashauri kutokupewa kibali cha ajira.

Malengo makuu ya idara ya ardhi na Maliasili ni kusimamimia na kutekelezaji sheria ya ardhi Na 4 ya mwaka 1999, sheria ya ardhi ya vijiji Na 5 ya mwaka 1999, sheria ya matumizi bora ya ardhi Na 6 ya mwaka 2007, sheria ya mipango miji Na 8 ya mwaka 2007, sheria ya misitu namba 14 ya mwaka 2002, sheria ya nyuki Na 15 ya mwaka 2002 na sheria ya wanyama pori Na 5 ya mwaka 2009 pamoja na taratibu, kanuni na miongozo yake. Katika kusimamia na kutekelezaji sheria hizi mambo mbalimbali yametekelezwa ikiwa ni pamoja na upimaji wa vijiji, upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ardhi, Kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya Miji, kumilikisha ardhi kwa waombaji, kuandaa mchakato wa kubatilisha hati miliki, utatuzi wa migogoro ya ardhi, ukusanyaji wa kodi ya pango utambuzi na usajili wa majengo kwaajili ya kulipa kodi ya majengo, na uthamini wa mali za Halmashauri kufanya ukaguzi/doria kwenye misitu ya asili vijijini na kando ya mito. Ukaguzi na uhakiki wa uvunaji wa mazao ya misitu hasa mbao na nguzo, ukusanyaji wa ushuru na ada za mazao ya misitu, ufuatiliaji wa vitalu vya miche ya miti na kutembelea na kutoa ushauri kwa wafugaji nyuki kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya.

.

I. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA IDARA

A. SEKTA YA ARDHI

1. UPIMAJI WA VIJIJI

Wilaya ya Ngara ina jumla ya vijiji 75. Kati ya hivyo Vijiji 60 vimepimwa na vina vyeti vya ardhi.Vijiji kumi na vitano (15) bado havijapimwa na havina Vyeti vya ardhi, Vijiji ambavyo havijapimwa na havina vyeti vya ardhi ni kutokana na kugawanywa kwa vijiji. Kati ya hivyo vijiji vipya ni 8 (Kigoyi, Kititiza, Kigina, Mshikamano, Nyakariba, Bulengo, Kyenda na Rwakalemera) na vijiji vya zamani ni 7 (Kasulo, Rusumo, Chivu, Nyamahwa, Mrukurazo, Nyakiziba Murubanga.)

2. UPANGAJI NA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MATUMIZI BORA YA ARDHI VIJIJINI

Vijiji 18 vimepanga mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuanza kutekeleza mipango hii. Katika utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, vijiji 10 vimejenga masijala za ardhi, mashamba 3286 yamepimwa na hati za kimila 3286 zimetolewa. Shughuli hizi zimefanyika kwa ufadhali wa Halmashauri ya Wilaya, Kagera TAMP, MKURABITA na shirika la CONCERN. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wataalam Kutoka makao makuu ya MKURABITA Kwa kusirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya na taasisi za fedha walitoa mafunzo kwa wananchi 220 wa Munjebwe na Buhororo kuhusu matumizi ya hati miliki za Kimila na jinsi ya kuomba na kurejesha mikopo. Kwa mwaka 2017/2018 hakuna kijiji kilichowezeshwa kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kutokana na makusanyo madogo ya Halmashauri ya Wilaya.

3. KUANDAA NA KUTEKELEZA MIPANGO YA MATUMIZI BORA YA ARDHI MIJINI

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ina maeneo yaliyotangazwa rasmi kuwa maeneo ya mipango miji kwenye gazeti la Serikali namba 176 la tarehe 09/08/1996.ambayo ni Mamlaka ya Mji Mdogo Rulenge, Mamlaka ya Mji Mdogo Ngara na Miji ya Rusumo, Benaco Kabanga, Murusagamba, Djululigwa, Kanazi, Mugoma na Muhweza. Katika miji hii ni eneo dogo sana ambalo limepangwa (town planning).kutokana na ukosefu wa fedha na uhaba wa wataalam

Halmashauri ina jumla ya viwanja 4012. Kati ya hivyo viwanja 1784 vimepimwa na kuwekewa alama za mipaka (vigingi). Viwanja vilivyopimwa mwaka wa 2017/2018 ni 42(Mkididiriviwanja 8 kitalu 'A' na 'C',Ngara Mjini viwanja 14 kitalu 'D' na 'G' NA Kasulo viwanja 20 kitalu 'E'.

Viwanja vyenye hati miliki ni 400. Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 viwanja 69 vimemilikishwa na rasimu 106 za hatimiliki zimeandaliwa.

Halmashauri imeandaa ramani 4 za mipango Miji Kwenye Miji ya Kabanga Rusumo Murusagamba na Ngara Mjini (Mkididiri) ambazo inatarajia kupima viwanja. Ramani ya mipango miji ya Rusumo ni muhimu kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa nguvu ya maji kwenye maporomoko ya Mto Kagera unaohusisha nchi tatu za Tanzania Rwanda na Burundi.

Ili kukabiliana na changamoto/tatizo la fedha na uhaba wa wataalam Halmashauri iko kwenye mchakato wa kuingia mkataba na Kampuni ya Mwanza Surveyors limited ili kuendelea kupanga miji yetu na kufanya upimaji shirikishi. Tayari vitongoji 4 vya Mamlaka ya Mji mdogo Ngara na Mji wa Benaco wamehamasishwa na kupewa elimu kuhusu upimaji shirikishi wa maeneo yao.

4. KUTOA HATI MILIKI KWA MASHAMBA MAKUBWA YANAYOZIDI EKARI 50

Waziri wa ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Vangimembe Lukuvikwenye ziara yake Wilayani Ngara Tarehe 22/02/2018 alitoa maagizo kwamba Wananchi wote wanahodhi ardhi kubwa (zaidi ya ekari 50) watume barua kwenye uongozi wa vijiji vyao kuomba kumilikishwa maeneo yao. Halmashauri kwa kutekeleza hili imetoa maagizo kwa vijiji vyote kuwataarifu wananchi kuandika barua za maombi ili mchakato uendelee. Kijiji cha Rwakalemera kimepata maombi na wanatarajia kufanya mkutano kujadili maombi hayo.

5. MASHAMBA MAKUBWA YENYE HATI MILIKI ZA SERIKALI KUU (KAMISHNA WA ARDHI)

Wilaya ya Ngara ina mashamba 7 yenye hati miliki zilizotolewa na Kamishna wa Ardhi. Katika ukaguzi uliofanyika mwaka 2017 mashamba 5 wamiliki wake walikiuka masharti yaliyoko kwenye hati miliki wakapewa ***ilani ya ubatilisho wa haki ya hati miliki***. Watatu walijitetea lakini mmoja anayejulikana kwa jina la Ndugu Abdallah Sadala hakupatikana na barua (Rejista) yake ilirudishwa ofisini na wafanyakazi wa Posta. Mmiliki huyu hajawahi kulipa kodi tangu apatiwe hati hiyo mwaka 1994, hajulikani aliko na hajawahi kufanya maendelezo ya aina yoyote. Hali hii ilipelekea wananchi wakijiji cha Rwakalemera kuvamia shamba hilo na kulima mazao mbalimbali. Kutokana na hali hiyo Hamashauri imepeleka mapendekezo ya kufutwa kwa umiliki wa shamba hili Kwa kamishna wa Ardhi ili mchakato uendelee.

Wamiliki waliopatiwa Ilani ya ubatilisho wa haki ya hati miliki ni kama ifuatavyo:

JINA LA MMILIKI	NA YA SHAMBA	UKUBWA WA SHAMBA	MAHALI LILIPO	HALI ILIVYOKUWA FEBRUARI 2018
Abdallah Sadallah	235	Ha 208.54 = ekari 521.3)	Rwakalemera	Hakuna mabadiliko. Halmashauri imepeleka mapendekezo ya kufuta umiliki wa shamba hili kwa Kamishna
Mushengezi Nyambele	745	Ha 198.95 = ekari 497.35	Rwakalemera	Wataalam walikwenda kuainisha mipaka kutokana na migogoro kati yake na kijiji.Ameshauriwa aendeleze shamba lake kulingana na mipaka yake
Mushengezi Nyambele	746	Ha 155.53 = ekari 388.83	Rwakalemera	Wataalam walikwenda kuainisha mipaka kutokana na migogoro kati yake na kijiji.Ameshauriwa aendeleze shamba lake kulingana na mipaka yake
Mahsen Saidi na Abdallah Saidi	333	Ha 183.2 =ekari 458	Rwakalemera	Wataalam, uongozi wa kijiji na kamati ya ardhi walikwenda kutambua shamba hili ili kuthibitisha utetezi wake lakini hakuweza kuonyesha mipaka yake.Hali hii imepelekea wataalam wakafufue mipaka na kuweka alama tena. Mmoja kati ya wamiliki hawa (Abdallah Saidi) alifariki dunia. Mahsein Saidi ameagizwa kufanya maendelezo kulingana na mipaka ya shamba lao na kulinda mipaka yake.
Dayosisi ya Kagera Ngara	696	Ha 36.12 = ekari 90.3	Ntobeye	Hawajalipa kodi

Kamishna wa Ardhi Kanda ya Ziwa akishirikiana na Wataalam wa Halmashauri walifanya tena ukaguzi wa mashamba haya mwezi Juni 2018 ili kuchukua hatua stahiki.

6. UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

Halmashauri kwa ushirikiano na ofisi ya Mkuu wa Wilaya tumekuwa tukifuatilia migogoro mbalimbali ya ardhi na kushirikiana na jamii kupata suluhu.Mwezi Februari 2018 takribani migogoro 150 iliwasilishwa kwa Mkuu wa Wilaya kwa Mtindo wa Fomu maalum ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi maarufu "Funguka kwa Waziri". Migogoro hii ilipitiwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenye ziara yake ya tarehe 22/02/2018. Baadhi ya matatizo yalipatiwa ufumbuzi na mengine yanaendelea kufanyiwa kazi.

7. **UKUSANYAJI KODI YA ARDHI:**

Mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya **Tshs 64,026,890/-** zilikusanywa na kuwasilishwa wizara ya ardhi.

Mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya **Tshs 59,672,817/-** zilikusanywa na kuwasilishwa wizara ya ardhi.

Mwaka wa fedha 2017/2018 tumekusanya jumla ya **Tshs 51,557,185/-**

8. UTAMBUZI NA USAJILI WA MAJENGO

Halmashauri ilifanya utambuzi na usajili wa majengo kwenye Mamlaka za miji midogo ya Ngara Mjini na Rulenge na Miji midogo ya Rusumo, Benaco, Kabanga na Mrusagamba kwa ajili ya kulipa kodi ya majengo. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilikuwa na lengo la kukusanya Tshs 40,000,000/- kutokana na kodi ya majengo na iliweza kukusanya zaidi ya Tshs27,000,000/- Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kodi ya majengo itakusanywa na Mamlaka ya mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority)

9. KUTHAMINI MALI ZA HALMASHAURI

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilifanya uthamini wa mali zake zinazotambulika kwa kumtumia Mtaalam wa uthamini kutoka Sengerema. Mali zinazotambulika na kufanyiwa uthamini zina thamani ya Tshs 53,026,466,819/-. Jedwali lifuatalo linaonesha kwa Muhtasari thamani ya mali za Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

S/N	AINA YA MALI	THAMANI YA MALI KABLA YA KUONDOA UCHAKAVU(TSHS)	THAMANI YA MALI BAADA YA KUONDOA UCHAKAVU (TSHS)
1.	ARDHI	1,952,896,250	1,952,896,250
2.	MAJENGO	49,728,285,450	31,085,847,740
3.	SAMANI	3,645,865,700	2,379,712,260
4.	VIFAA NA MITAMBO	1,189,455,800	899,533,620
5.	PIKIPIKI	418,000,000	242,400,000
6.	MAGARI	3,039,400,000	1,786,860,000
7.	MIUNDOMBINUYA MAJI	7,663,473,013	4,892,601,949
8.	MTANDAO WA BARABARA	13,261,390,000	9,786,615,000
	JUMLA	80,898,966,213	53,026,466,819

KITENGO CHA MALIASILI

1. MISITU:

Katika kutekeleza malengo ya kitaifa ya kupandaji miti 1,500,000 kila mwaka, Halmashauri imefanikiwa kupanda jumla ya miti 6,024.923 sawa na asilimia 67% kwa kipindi cha miaka 6. Mafanikio haya ni kutokana na hamasa kubwa ya wananchi kuotesha miche ya miti ya mbao na matunda kwa ajili ya biashara.

Katika Halmashauri kuna vitalu zaidi ya 20 vya vikundi na watu binafsi. Idara inatembelea bustani hizi kutoa ushauri wa kitaalam wa kutunza vitalu. Aidha halmashauri inatoa elimu ya upandaji miti kwa vikundi na watu binafsi.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wataalam walikwenda kwenye vijiji 36 vyenye miradi ya upandaji miti vinavyofadhiliwa na TASAF kutoa ushauri na elimu ya upandaji miti kwa kaya maskini ambazo ziko kwenye mpango wa TASAF wa kuwanusuru na umaskini. Vijiji hivyo ni Mukibogoye, Mayenzi, Katerere, Djuliligwa, Kanyinya, Murubanga, Ntanga, Magamba Mukalinzi,Mumuhamba, Buhororo, Nyamiaga, Murutabo, Kabalenzi, Muruvyagira, Nyamahwa, Mubuhenge,Murubanga, Kasharazi Mukibogoye, Mugoma, Kasange, Kigina, Rwinyana, Nterungwe, Mukubu, Nyabisindu, Kasulo, Ruzenze, Mwivuza, Murutabo, Kazingati Nyabihanga, Magamba na Kumuzuza.

2. NYUKI:

Lengo la sekta hii ni kuboresha ufugaji wa nyuki na kupanua wigo ili kuinua kipato cha wananchi, kuongeza lishe na kuchangia hifadhi ya misitu na mazingira kwa ujumla. Kwa takwimu za mwaka 2017/2018 vikundi vya wafugaji wa nyuki vinavyojulika ni 8.Jumla ya mizinga ya kisasa ya vikundi na watu binafsi ni 1615 na mizinga ya kienyeji ni 4829.

Halmashauri imetenga fedha karibu Tshs 300,000,000/- kupitia mradi wa kufua umeme wa maji Rusumo kwa ajili ya kutoa elimu ya ufugaji bora wa nyuki na uvunaji wa asali.

3. **WANYAMAPORI:**

Wilaya ya Ngara imepakana na Hifadhi za wanyamapori Burigi na Kimisi ambapo wanyamapori hasa tembo wana tabia ya kuondoka mbugani na kufanya uharibifu kwenye mashamba ya wananchi kwenye vijiji vya Kasulo, Rusumo, Murubanga na Kumubuga. Aidha kuna uvamizi wa makundi makubwa ya ngombe kwenye hifadhi hizi hasa kutoka nchi jirani. Hivyo Halmashauri kwa kushirikiana na askari wa hifadhi hizi na kamati za ulinzi na usalama Mkoa na Wilaya hufanya doria za mara kwa mara kudhibiti hali hii.

Aidha Halmashauri kwa kushirikiana na Mali Hai Clubs of Tanzania na wataalam wa mapori ya akiba ya Burigi na Kimisi walihamasisha na kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yao. Mafunzo haya yalifanyika tarehe 19/01/2018 – 02/02/2018 ambapo mikutano 27 iliyohusisha shule 19 na vijiji 8 Mikutano hiyo ilihudhuriwa na jumla ya watu 10,283 wakiwemo waalimu 208, wanafunzi 9,042 na wanavijiji 1,033. Aidha wanafunzi walihamasishwa kuanzisha vikundi vya Malihai Clubs kwenye shule zao kwa lengo la kujifunza uhifadhi wa maliasili na mazingira. Vijiji na shule zilizoshiriki mafunzo zinaokena kwenye majedwali yafuatayo:

VIJIJIVILIVYOTEMBELEWA NA IDADI YA WASHIRIKI WA MAFUNZO

S/N	JINA LA KIJIJI	IDADI YA WASHIRIKI WA MAFUNZO
1.	Kasulo – Ngoma	124
2.	Rwakalemera - Kamuli	91
3.	Nyakariba	153
4.	Rusumo	0
5.	Mshikamano	120
6.	Kasharazi	0
7.	Kigina	268
8.	Mayenzi	118
9.	Katerere	24
10.	Mukarehe	135
	JUMLA	**1033**

SHULE ZILIZOTEMBELEWA NA IDADI YA WASHIRIKI WA MAFUNZO

S/N	JINA LA SHULE	IDADI YA WANAFUNZI WALIOSHIRIKI MAFUNZO	IDADI YA WAALIMU WALIOSHIRIKI MAFUNZO
1.	S/M Ngoma	640	12
2.	S/M Kasuko	547	10
3.	S/S Rusumo	562	26
4.	S/M Kapfuha	413	11
5.	S/M Njiapanda	530	11
6.	S/M Kamuli	402	9
7.	S/M Kumunazi	1503	7
8.	S/M Kabaheshi	644	11
9.	S/M Nyakahanga	240	10
10.	S/S Rusumo B	315	10
11.	S/M Rusumo Magereza/ Mshikamano	336	9
12.	S/M Kasharazi	615	6
13.	S/M Ntobeye	362	12
14.	S/M Kigina	250	8
15.	S/S Kibimba	338	17
16.	S/M Mayenzi	365	14
17.	S/M Katerere	350	6
18.	S/S Kanazi	400	13
19.	S/M Mukarehe	230	6
JUMLA		**9042**	**208**

4.KUKUSANYA USHURU WA MAZAO YA MISITU

Ili kuhakikisha kunakuwepo na tija na ufanisi wa ulipaji wa ushuru wa mazao ya misitu wataalam walitembelea makarakana yaliopo maeneo ya Ngara mjini na kuwakumbusha suala la ulipaji wa ushuru. Pia tuliwafundisha ujazaji wa daftari la kumbukumbu ya mazao ya misitu ili kurahisisha ukusanyaji wa ushuru. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 idara imekusanya mapato ya mazao ya misitu kiasi cha Tshs 12,274,800/-. Kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na miaka iliyopita kwa mfano mwaka 2016/2017 tulikusanya jumla ya Tshs. 30,119,750/- Hali hii imetoka na udhibiti mzuri wa uvunaji holela wa misitu uliokuwa unafanyika kwa ajili ya kuchoma mkaa.

CHANGAMOTO:

1. Ukosefu wa fedha. Mipango na bajeti inayopangwa haitekelezeki kutokana na kutoletewa fedha zilizoidhinishwa. Aidha hatuletewi fedha za retention kama wilaya nyingine.
2. Uhaba wa watumishi katika sekta. Sekta ina wataalam 02 tu wa ardhi (Afisa ardhi msaidizi 01 na Msanifu ramani msaidizi 01.)

3. Ukosefu wa usafiri wa uhakika. Shughuli za ardhi hususani utatuzi wa migogoro zinahitaji usafiri wa uhakika lakini sekta haina usafiri wa aina yoyote.

4. Kasi ndogo ya kupanga mipango Miji yetu. Hali hii imesababishwa na uhaba wa wataalam na Halmashauri kutokuwa na uwezo wa kulipa fidia kwa wenye maeneo baada ya kuandaa TP.

B. JINSI TUNAVYOKABILIANA NA CHANGAMOTO HIZI

1. Wadau wengine wa maendeleo wanagharamia shughuli mbalimbali za ardhi kwa mfano shirika la CONCERN waligharamia upimaji wa mashamba na maandalizi ya hati miliki za kimila kwa familia maskini. NELSAP wamegharamia maandalizi ya TP Rusumo pamoja na kuweka alama za mipaka.Aidha wameahidi kugharamia upimaji wa viwanja na mashamba ya watu walioathiriwa na mradi .

2. Kwa suala la uhaba wa watumishi tunao wataalam wa kujitolea 2 (Mpima 01 na msanifu wa ramani 01). Aidha tunatumia wanavyuo kutoka vyuo vya ardhi Tabora,UCLAS, Morogoro na Mbezi wakati wakiwa Likizo. Pia wakati mwingine inatubidi kuazima wataalam kutoka wilaya jirani. Aidha Halmashauri iko kwenye mchakato wa kuingia mkataba na Kampuni ya Mwanza Surveyors limited ili kupanga Miji yetu na kufanya upimiji shirikishi wa viwanja.

3. Tunaomba usafiri kwenye idara nyingine.

4. Tumehamasisha/tunaendelea kuhamasisha jamii ili waruhusu ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya jamii kwenye maeneo yenye TP kwa ridhaa yao bila kudai fidia.